BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2019

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2019

# 015 – ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P. 2624,

Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


YALIYOMO ........ iii

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA ........ 2

2.1 SEHEMU (A) ........ 2

2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Majibu Sahihi. ........ 2

2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha ........ 8

2.2 SEHEMU B: Maswali ya kujibu kwa ufupi ........ 10

2.2.1 Swali la 3: Familia ya kiislamu. ........ 10

2.2.2 Swali la 4: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu ........ 13

2.2.3 Swali la 5: Nguzo za Imani ........ 15

2.2.4 Swali la 6: Nguzo za Uislamu ........ 18

2.2.5 Swali la 7: Mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu. ........ 20

2.2.6 Swali la 8: Qur`an ........ 23

2.2.7 Swali la 9: Sunnah na Hadithi ........ 26

2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha ........ 29

2.3.1 Swali la 10: Dola ya Kiislamu Madinah ........ 30

2.3.2 Swali la 11: Qur'an. ........ 36

2.3.3 Swali la 12: Nguzo za Uislamu ........ 42

2.3.4 Swali la 13: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu ........ 47

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA KILA MADA ........ 54

4.0 HITIMISHO ........ 55

5.0 MAPENDEKEZO ........ 55

6.0 Kiambatisho ........ 56

# DIBAJI

Taarifa hii ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2019 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kuhusu kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa somo hili. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Katika taarifa hii, uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza katika majibu ya maswali zimeainishwa kwa kuonesha watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi. Pia uchambuzi huu umeonesha watahiniwa waliopata alama za juu, wastani na chini katika kila swali na sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri au vibaya zimeoneshwa. Aidha, sababu mbalimbali ambazo zilichangia wanafunzi kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi zimeelezwa. Sababu zilizowafanya baadhi ya wanafunzi kuweza kujibu maswali kwa usahihi ni kama vile uelewa wa matakwa ya maswali na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na kutotambua matakwa ya maswali na kuwa na maarifa finyu katika mada mbalimbali na hasa katika Mambo ya lazima kufanyiwa maiti ya Kiislamu na Nguzo za Imani. Uchambuzi umebaini kuwepo kwa udhaifu katika kujibu maswali ya kujibu kwa ufupi na yale ya kujieleza kwa insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili hatimaye kuondoa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii. Endapo mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa uchambuzi huu yatafanyiwa kazi, ujuzi na maarifa watakaopewa wanafunzi wa kidato cha nne katika somo hili utaongezeka na kiwango cha kufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha kufaulu katika mtihani wa kidato cha nne (CSEE) wa mwaka 2019, somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani huo uliofanyika mwezi novemba 2019 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo hili kwa kidato cha I hadi IV wa mwaka 2012.

Mtihani huu ulikuwa na karatasi moja iliyokuwa na sehemu tatu: A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na tatu. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili. Swali la kwanza lilikuwa na vipengele kumi na tano (i-xv) ambapo mtahiniwa alitakiwa kuchagua majibu sahihi, swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha lenye vipengele vitano (i-v) nalo lilikuwa na jumla ya alama 5. Sehemu B ilikuwa na maswali saba (7) ya kujibu kwa ufupi. Kila swali lilibeba alama 5 kwa hiyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 35. Sehemu C ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu tu, kila swali lilikuwa na alama 15 na kuifanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 45. Jumla ya alama zote katika karatasi hii zilikuwa 100.

Idadi ya watahiniwa walioandikishwa kufanya mtihani wa Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2019 ni 69,433 na waliofanya mtihani walikuwa 67,230. Hii ni sawa na ongezeko la watahiniwa 20,361 ikilinganishwa na watahiniwa 46,869 waliofanya mtihani wa Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2018. Aidha, watahiniwa 67,035 walipata matokeo ambapo watahiniwa 36,565 sawa na 54.55% walifaulu. Kati ya hawa, watahiniwa 20 (0.05%) walipata gredi A, 407 (1.11%) walipata gredi B, 11,123 (30.42%) walipata gredi C na 25,015 (68.41%) walipata gredi D. Watahiniwa 30,470 sawa na asilimia 45.45 walipata gredi F. Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2019 kilikuwa asilimia 54.55.

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa maswali ya mtihani na majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimewekwa ili kuonesha kile kilichofanywa na watahiniwa. Kufaulu kwa watahiniwa kuligawanyika katika mafungu matatu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Kufaulu kwa mada kulikuwa dhaifu kama kulikuwa kati ya asilimia 0 hadi 29. kufaulu kulikuwa wastani kama kulikuwa kati ya asilimia 30 hadi 64 na kufaulu kulikuwa vizuri kati ya asilimia 65 hadi 100.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA MADA


### 2.1 SEHEMU (A)

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili na ilikuwa na jumla ya alama 20. Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi ambapo mtahiniwa alipewa sentensi yenye majibu matano ya kuchagua (A, B, C, D na E) na kutakiwa kuchagua herufi moja ya jibu sahihi na kujaza katika karatasi yake ya kujibia. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha ambapo mtahiniwa alitakiwa aoanishe matendo matano yaliyopo katika orodha A (i - v) na majina ya matendo hayo katika orodha B (A hadi G) na kujaza katika kitabu chake cha kujibia.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Majibu Sahihi

Swali la kwanza lilikuwa na vipengele kumi na tano (i-xv). Miongoni mwa mada zilizopimwa katika swali hili zilikuwa ni: (i) Dola ya Kiislamu Madinah, (ii) Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w), (iii-v) Sunnah na Hadithi, (vi-ix) Qur'an, (x) Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, (xi - xii) Familia ya Kiislamu, (xiii) Sheria katika Uislamu na (xiv - xv) Nguzo za Imani. Katika kila kipengele mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya majibu matano (A-E) aliyopewa na kuandika herufi ya jibu hilo katika kitabu chake cha kujibia. Kila kipengele kilikuwa na alama 1, hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 67,199 (99.84%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 64,122 (95.46%) walifaulu. Watahiniwa 38,304 (57.00%) walipata alama za wastani (5 hadi 9), na watahiniwa 25,818 (38.42%) walipata alama za juu (10 hadi 15), ambapo kati yao watahiniwa 181 walipata alama zote 15 za swali hili. Watahiniwa 3,077 (4.58%) walipata alama za chini (0 hadi 4) ambapo miongoni mwao watahiniwa 47 walipata alama 0. Chati namba 1 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hawa kwa asilimia.




***Chati ya 1**: Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 1*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 64,122 (95.46%) kati ya 67,199 waliojibu swali hili walipata alama 5 hadi 15. Watahiniwa waliopata alama za wastani (5 hadi 9) waliweza kujibu vizuri vipengele vitano hadi tisa vya swali na wale waliopata alama za juu (10 hadi 15) walijibu vizuri vipengele kumi na zaidi kati ya vipengele kumi na tano vya swali. Miongoni mwa vipengele vilivyojibiwa vizuri na watahiniwa hawa ni; (iii, iv, v, vi, vii, ix, x, xi na xv) vilivyotoka katika mada za: Sunnah na Hadithi, Qur`an, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Familia ya Kiislamu na Nguzo za Imani. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawa walielewa vema vipengele hivyo na walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada hizo, hivyo walifanya vizuri. Watahiniwa waliopata alama za chini (0 hadi 4 ) walishindwa kuchagua majibu sahihi katika vipengele vingi vya swali kutokana na sababu mbalimbali kama zinavyochambuliwa katika aya zinazofuata;

Kipengele cha (i) kilitoka katika mada ya "Dola ya kiislamu Madinah" katika mada ndogo ya "Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Madinah". Katika kipengele hiki watahiniwa walitakiwa kuchagua kundi linaloonesha vyanzo muhimu vya mapato katika serikali ya Kiislamu ambapo jibu sahihi lilikuwa ni E *(Zakat, Sadaka, Jizya, Al kharaj, Al-fay, Al-ghanimah na Al-ushru)*. Watahiniwa wengi hawakuwa na ufahamu juu ya istilahi hizi, hivyo

hawakuweza kuchagua jibu sahihi. Wengine hawakuweza kuchagua jibu sahihi kutokana na kutokuwa na ufahamu juu ya mada husika kwa ujumla na hatimae walishindwa kufanya vizuri.

Kipengele cha (ii) kilitoka katika mada ya Historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w) kipengele hiki kiliuliza sababu ya baadhi ya watu kuasi Uislamu mara baada ya kutawafu kwa Mtume (s.a.w), jibu sahihi lilikuwa ni B (*uroho wa madaraka*). Watahiniwa wengi walijibu kwa usahihi. Watahiniwa waliokosa kipengele hiki walichagua jibu A *(kukataa kutoa zaka)* jibu linaloonesha kuwa watahiniwa hawa walichanganya majibu kutokana na kuwa na maarifa finyu. K*ukataa kutoa Zaka* ni matokeo ya uasi. Watahiniwa wengine walichagua jibu C *(ugumu wa sharia za kiislamu)* kwa sababu ya kutokuwa na maarifa ya kutosha.

Kipengele cha (iii) kilitoka katika mada ya "Sunnah na Hadithi", katika mada ndogo ya Uchambuzi wa Hadithi za Mtume (s.a.w). Kipengele hiki kiliuliza kuhusu kanuni inayotumika kuchuja Hadithi za Mtume (s.a.w) na jibu lake sahihi lilikuwa D (*kwa kuangalia maisha ya wapokezi wa Hadithi*). Uchambuzi unaonesha watahiniwa wengi hawakuchagua herufi sahihi na badala yake walichagua E (*kuangalia matumizi ya hadithi hiyo katika maisha*) kwa sababu hawakuwa na uelewa wa kanuni zinazotumika kuchuja Hadithi za Mtume (s.a.w) hivyo watahiniwa hao walibahatisha majibu kwa kuuganisha mzizi wa swali na kila jibu lililopo ikizingatiwa kuwa jibu E lilikuwa na muunganiko mzuri kilugha.

Kipengele cha (iv) kilitoka katika mada ya "Sunnah na Hadithi" katika mada ndogo ya Tanzu za Hadithi. Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuchagua kundi ambalo litawekwa Hadithi iliyosimuliwa na msimulizi anayejulikana kuwa na uwezo mdogo wa kuhifadhi masimulizi. Jibu sahihi lilikuwa ni A *(dhaifu).* Takwimu zinaonesha wengi walijibu kwa usahihi na wachache waliokosa walichagua jibu C *(Maudhuu).* Waliokosa kipengele hiki hawakuwa na maarifa ya kutosha katika uchambuzi wa Hadithi, hivyo walishindwa kubaini vigezo vya Hadithi dhaifu.

Kipengele cha (v) pia kilitoka katika mada ya "Sunnah na Hadithi". Mtahiniwa alitakiwa kuainisha kundi la Hadithi linalotokana na Isnad *(msururu wa wapokezi)* ya watu wema na waadilifu katika maisha yao. Jibu sahihi lilikuwa ni E *(sahihi)*. Watahiniwa wengi waliweza kuchagua jibu

hili kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya uchambuzi wa Hadithi. Watahiniwa wengi waliokosa walichagua jibu A. Watahiniwa hawa walionesha kuwa hawafahamu maana ya neno “Maudhuu” katika fani ya Hadithi.

Kipengele cha (vi) kilitoka katika mada ya Qur`an na kilimtaka mtahiniwa kuainisha mafunzo ya Suratul Fatiha endapo Muislamu anataka kuanza kufanya jambo lolote lile. Jibu sahihi lilikuwa B (*kusoma Bismillahi Rahmani Rahiim*. Watahiniwa wengi walijibu kwa usahihi kwakuwa kusoma Bismillahi Rahmani Rahiim ni kitendo ambacho kimezoeleka kufanywa na waumini wa Kiislamu katika maisha yao ya kila siku kabla ya kufanya jambo lolote. Baadhi ya watahiniwa waliokosa kipengele hiki walichagua jibu A. Hii ni kwa sababu ya mafundisho kuwa kabla ya kuanza kusoma Qur’an msomaji anatakiwa kuanza kwa kumlaani shetani kwa kutamka Audhubillah Mina Shaytwaanir Rajiim.

Kipengele cha (vii) kilihusiana na mada ya Qur`an katika mada ndogo ya “Surah zilizochaguliwa”. Swali lilimtaka mtahiniwa ataje dhambi kubwa inayotajwa katika suratul Humazah. Jibu sahihi lilikuwa ni B (*kusengenya*). Watahiniwa wengi walifanya vizuri katika kipengele hiki. Inaonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya tafsiri ya suratul Humazah. Watahiniwa waliokosa kipengele hiki walikuwa hawajui maudhui ya Suratul Humazah, hivyo majibu yao yalikuwa ya kubahatisha.

Kipengele cha (viii) kilitoka kwenye mada ya Qur`an, mafunzo ya Surah zilizoteuliwa “Suratul Bayyinah”. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha tafsiri ya aya ya saba ya sura hiyo. Jibu sahihi lilikuwa B (*hakika wale walio amini na kutenda mema basi hao ndio wema wa viumbe*). Kufaulu katika kipengele hiki kulikuwa ni kwa wastani. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa wamehifadhi surat Bayyinah na walikuwa wanafahamu vizuri tafsiri yake. Watahiniwa wengi waliokosa swali hili walichagua jibu C (*ndani yake kuna sharia madhubuti*) na D (*kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema {mlizopewa}*). Watahiniwa hawa hawakuwa wanafahamu “Suratul Bayyinah” katika matini na tafsiri yake.

Kipengele cha (ix) kilipima mada ya Qur`an katika kipengele cha adabu za usomaji wa Qur`an. Mtahiniwa alitakiwa kubaini katika Orodha ya adabu zilizoorodheshwa ni ipi haikuwa miongoni mwa adabu za usomaji wa Qur`an. Jibu sahihi lilikuwa ni C (*kuanza kwa sauti ya chini kisha kwa sauti ya juu katika kusoma*). Watahiniwa wengi walifanya vizuri katika kipengele hiki. Hii inadhihirisha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu adabu za usomaji wa Qur`an. Waislamu wengi huzingatia adabu mbalimbali za usomaji wa Qur'an katika usomaji wao wa kila siku. Hivyo nyingi katika adabu hizi zimezoeleka na hufuatwa na wasomaji wa Qur'an. Hata hivyo katika kipengele hiki wapo waliochagua majibu mengine ambayo si sahihi. Watahiniwa hawa walionesha kutokuelewa swali na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Adabu za kuisoma Qur`an.

Kipengele cha (x) kilipima mada ya "Mtazamo wa Uislamu juu ya dini". Kwenye kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu linaloonesha kazi kuu ya dini kwa mtazamo wa Uislamu. Watahiniwa wengi walifanya vizuri katika kipengele hiki kwa kuchagua jibu sahihi ambalo lilikuwa ni A (*kusimamia sheria na kumkomboa mwanadamu*). Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya kazi ya dini kwa mtazamo wa Uislamu. Hata hivyo majibu B, D na E hayakuchaguliwa kwa vile yalitaja mambo ambayo yapo kinyume na Uislamu.

Kipengele cha (xi) kilitoka katika mada ya "Familia katika Uislamu". Mtahiniwa alitakiwa kubaini jinsi ndoa inavyomuhifadhi Muislamu kutokana na zinaa. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa ni C (*imeweka utaratibu madhubuti wa kukidhi haja*). Watahiniwa wengi walimudu kuchagua jibu sahihi katika kipengele hiki kwa sababu ndoa ni ibada muhimu katika jamii. Watahiniwa walionesha kuwa na maarifa ya ziada kuhusu mada hii. Baadhi ya watahiniwa ambao hawakulielewa swali walijibu kipengele hiki kwa kubahatisha.

Kipengele cha (xii) kilitoka katika mada ya "Familia ya Kiislamu" katika mada ndogo ya "Talaka na Eda". Kipengele hiki kiliuliza kuhusu hukumu ya mwanamke mjamzito aliyepewa talaka katika sheria ya kiislamu. Jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa ni E (*eda hadi pale atakapo jifungua*). Watahiniwa wengi walimudu kuchagua jibu sahihi katika kipengele hiki, kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Talaka na Eda. Baadhi ya waliokosa kipengele hiki walichagua jibu D (*eda hadi atakapo maliza*

*kunyonyesha*) ambalo halikuwa jibu sahihi. Ama watahiniwa wengine waliochagua majibu A, B na C wote walidhihirisha kutokuwa na marifa ya kutosha juu ya mada ya talaka na eda.

Kipengele cha (xiii), kilitoka katika mada ya "Sheria katika Uislamu" kipengele hiki kiliuliza kuhusu adhabu ya mlevi katika sharia ya Uislamu. Jibu la swali hili lilikuwa ni D (*kuchapwa viboko arobaini*). Watahiniwa wengi walimudu kuchagua jibu sahihi hali iliyoonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada hii ya Sheria katika Uislamu. Hata hivyo wapo baadhi ya watahiniwa walichagua majibu mengine kama vile A, C na E kwa sababu mbalimbali: Waliochagua A (*kuchapwa viboko mia moja*) hawa walishindwa kutofautisha kati ya adhabu ya mlevi na mzinifu, wale waliochagua C (*kuchwapwa viboko hamsini*) na E (*kuchapwa viboko ishirini na moja*) walionesha kuwa hawana maarifa yakutosha juu ya hukumu za kisheria zilizoainishwa katika Uislamu kwa makosa ya ulevi hivyo walichagua majibu yao kwa kubahatisha.

Kipengele cha (xiv), kilitoka katika mada ya "Nguzo za Imani" katika kipengele cha "kuamini siku ya mwisho". Kipengele hiki kiliuliza kuhusu maana sahihi ya kuamini siku ya mwisho ambapo jibu lake sahihi lilikuwa ni B (*kuna maisha ya milele baada ya kufufuliwa*). Kufaulu kwa watahiniwa katika kipengele hiki kulikuwa kuzuri kwani watahiniwa wengi waliweza kuchagua jibu hilo kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mada ya Imani ya siku ya mwisho. Watahiniwa wachache walichagua majibu ambayo hayakuwa sahihi kama vile C (*unapokufa nchi moja utafufuliwa nyingine*) na wengine D *(haiwezekani kufufuliwa tena baada ya kufa*). Watahiniwa hawa walionesha kuwa wameathiriwa na imani kuwa mtu akifa sehemu moja ya dunia hufufuliwa kwa kuzaliwa tena upya sehemu nyingine. Watahiniwa wengine walijibu kwa mtazamo wa makafiri kuwa hakuna maisha baada ya kufa.


Kipengele cha (xv) kilitoka katika mada ya Nguzo za Imani katika kipengele cha Kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu. Katika kipengele hiki watahiniwa walitakiwa kubaini sababu ya kuhitajika Mtume mwingine baada ya Mtume wa kwanza kurejea kwa mola wake. Jibu sahihi lilikuwa ni D (*Mtume aliyetangulia alipelekwa kwa taifa maalum*). Kufaulu kwa watahiniwa katika kipengele hiki kulikuwa kwa wastani.

Baadhi ya watahiniwa walichagua jibu B (*Mtume aliyefuata alikuwa na mafundisho tofauti na aliyetangulia*), watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa misingi ya mafundisho ya mitume haitofautiana. Watahiniwa wachache walichagua majibu A, C na E ambayo hayakuwa majibu sahihi. Majibu haya yanaashiria kuwa watahiniwa hawa hawakuwa na ufahamu kuhusu mada husika hivyo walikuwa wanabahatisha.

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali hili lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu, mada ndogo ya Hija na Umrah. Mtahiniwa alitakiwa kuoanisha matendo ya Hija yaliyokuwa katika orodha A (i-v) na majina ya matendo hayo kutoka orodha B (A-G) na kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kitabu cha kujibia.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 67,124 (99.70%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 30,672 (45.70%) walipata alama 0 hadi 1 katika swali hili. Watahiniwa 27,242 (40.58%) walipata alama 2 hadi 3 na watahiniwa 9,210 (13.72%) walipata alama 4 hadi 5. Chati namba 2 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hao kwa asilimia.




***Chati ya 2****: Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 2*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili ni cha wastani kwani watahiniwa 36,452 (54.31%) waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 5. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu ibada ya Hija na Umra jambo ambalo liliwawezesha kuoanisha kwa usahihi vipengele vingi na wengine vyote vya swali hili. Vipengele ambavyo kwa kiasi kikubwa watahiniwa hawa walimudu kuvioanisha kwa usahihi ni: (i), (iii) na (v). Hii ni kwa sababu Mahujaji huvirejea vitendo hivi kwa kuvitaja kwa majina kila wanapoeleza namna walivyotekeleza ibada ya Hija.

Kipengele cha (i) chenye sentensi inayosema "mahujaji husimama, kuleta dhikri na kuomba dua mchana kutwa " ni miongoni mwa vipengele ambavyo watahiniwa walifanya vizuri. Jibu la kipengele hiki lilikuwa ni herufi D (Arafa). Tukio la mahujaji kusimama Arafa linakumbukwa sana na waumini ambao hawakwenda Makka kufanya ibada ya Hija ili waweze kutekeleza Sunnah ya kufunga inayoambatana na siku hiyo. Watahiniwa ambao hawakuoanisha kipengele hiki kwa usahihi, wengi walioanisha na herufi G (miqaat) ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa hawa walihusisha neno miqaati na "mahujaji kusimama" kwasababu miqaat ni sehemu au vituo ambavyo mahujaji husimama kwa ajili ya kutia nia ya Hija na kuvaa ihram ili kuendelea na hatua nyingine.

Katika kipengele cha (iii) chenye sentensi inayosema "mahujaji hutembea mara saba baina ya safwa na marwa" pia ni miongoni mwa vipengele ambavyo watahiniwa walifanya vizuri. Jibu la kipengele hiki lilikuwa ni F (sa`i). Watahiniwa walioshindwa kuonanisha kipengele hiki kwa usahihi waliweka majibu ya kubahatisha. Baadhi yao walioanisha na herufi C (Tawafu) kwa sababu kitendo cha Tawafu hufanyika mara saba kama ilivyo kitendo cha (sa`i), hivyo majibu yaliwachanganya.

Kipengele cha (v) chenye sentensi isemayo "mahujaji huzunguka al-kaaba mara saba kuanzia jiwe jeusi" ni miongoni mwa vipengele ambavyo watahiniwa wengi walimudu kuonanisha kwa usahihi. Jibu la kipengele hiki lilikuwa ni C (Tawafu). Watahiniwa ambao hawakuonanisha kipengele hiki kwa usahihi walichagua herufi E (Qiraan) na wengine A (ifraad) kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kufahamu kuwa hizo zilikuwa ni aina za Hija.

Uchambuzi zaidi katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa vipengele ambavyo watahiniwa wengi hawakufanya vizuri ni (ii na iv). Katika kipengele cha (ii) kinachosema mahujaji hutia nia ya hija na kuvaa ihram, jibu lake lilikuwa G (Miqaat). Watahiniwa wachache waliweza kuoanisha kipengele hiki kwa usahihi. Watahiniwa wengine walioanisha kipengele hiki na herufi A (Ifraad) kwa sababu kitendo hiki cha kutia nia na kuvaa Ihram katika Miqaat hakipewi uzito mkubwa katika mafundisho ya ibada ya Hija pia watahiniwa kutojua maana ya neno "infraad" hivyo wakabahatisha ili kuona kama yanaendana.


Kipengele cha (iv) kiliwataka watahiniwa kubaini Hija iliyo nafuu kwa mahujaji wanaotoka mbali na Makka. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa B (Tamattu). Watahiniwa wengi walishindwa kuonisha kwa usahihi kwa sababu ya kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za Hija na kukosa uzoefu kutoka kwa watu waliowahi kuhudhuria ibada hii.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya kujibu kwa ufupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi ambayo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama tano (5) hivyo jumla ya alama zote katika sehemu hii ilikuwa 35. Maswali katika sehemu hii yalitoka katika mada zifuatazo: Familia ya kiislamu, Mfumo wa jamii ya Kiislamu, Nguzo za Imani, Nguzo za Uislamu, Mambo ya lazima ya kufanyiwa maiti Muislamu, Qur`an na Sunnah na Hadithi.

### 2.2.1 Swali la 3: Familia ya Kiislamu.

Swali hili lilitoka katika mada ya Familia katika Uislamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa ufupi kwa nini mwanamke wa kiislamu haruhusiwi kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja. Swali lilijibiwa na watahiniwa 64,952 (96.50%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 42,737 (65.80%) walipata alama 0 hadi 1 za swali hili. Watahiniwa 20,206 (31.11%) walipata alama 1.5 hadi 2.5 na watahiniwa 2,009 (3.09%) walipata alama 3.5 hadi 5. Chati namba 2 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hawa katika asilimia.





***Chati ya: 3:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 3*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa ni wastani, kwa kuwa watahiniwa 22,215 (34.20%) kati ya 64,952 waliojibu swali hili walipata alama 1.5 hadi 5. Watahiniwa 20,206 (31.11%) walipata alama za wastani (1.5 hadi 3) na watahiniwa 2,009 (3.09%) walipata alama za juu (3.5 hadi 5). Watahiniwa 20,206 (31.11%) waliopata alama za wastani hawakuweza kutoa ufafanuzi wa kutosha kwenye hoja walizozitoa kuelezea sababu za Uislamu kukataza mwanamke kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja ingawa hoja zao zilikuwa sahihi.


Watahiniwa waliopata alama za juu (3.5 hadi 5) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada hii ya Familia ya Kiislamu. Vile vile walielewa vema matakwa ya swali na waliweza kutoa hoja madhubuti na kufafanua kwa usahihi kwanini mwanamke wa kiislamu haruhusiwi kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja. Ufafanuzi waotoa ulijumuisha hoja kama vile: *mwanamke atakapopata mimba mtoto hatafahamika baba yake wa halali, Kwa hali hii mtoto atakoseshwa haki zake za msingi ikiwemo nasaba, malezi ya baba na mirathi. Mtoto huyu anaweza kuchukua mirathi isiyo haki yake. Itakuwa ni ngumu mwnamke huyu kutekeleza majukumu ya mke kwa mume ikizingatiwa kuwa mume ni kiongozi katika familia. Matokeo ya hali hii itakuwa ni migogoro katika*

*jamii*. Kielelezo namba 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


3. Mwanamke wa kislamu haruhusiwi kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja kwasababu mwanamke yeye ndiye anayebeba ujauzito hivyo akiwa na mwanamume zaidi ya mmoja ujauzito utakuwa hauna mume na hata mtoto atakayezaliwa atakuwa hana baba halisia. Hivyo itazua ugomvi baina ya wanaume wengi wenye mke mmoja.

Kielelezo 3.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 3

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 42,737 (65.80%) walipata alama za chini (0 hadi 1), miongoni mwao watahiniwa 32,235 (47.90%) walipa alama 0. Watahiniwa hawa walijibu tofauti na matakwa ya swali kwa sababu ya kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya kipengele kilichoulizwa hivyo wakapata alama 0. Baadhi yao walikuwa wakirejea msingi wa swali kuwa: *Mwanamke wa kiislamu haruhusiwi kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja kwa sababu dini ya kiislamu hairuhusu,* na majibu mengine yanayofanana na hayo kama vile: *Dini yetu ya kiislamu haijaeleza kuwa mwanamke wa kiislamu aolewe na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja, mwanamke haruhusiwi kuolewa akiwa ndani ya ndoa, dini ya Kiislamu hairuhusu, Qur'ani hairuhusu, kwa sababu hiyo ni sheria ya Uislamu, kwa sababu Allah (s.w) amejaalia aolewe na mume mmoja.* Wengine walitoa hoja moja kuwa*: Mwanamke hawezi kuwahimili wala kuwatosheleza wanaume wawili kwa wakati mmoja wala kutekeleza majukumu, mwanamke ameumbwa dhaifu hivyo hana uwezo wa kumudu mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.* Kielelezo namba 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kama ilivyotakiwa.



3 Kwa sababu mwanamke wa kiislamu hawezi kuwahudumia wanaume wawili kwa wakati mmoja pia hiyo itakuwa ni ubakaji. Ndio maana mwanamke wa kiislamu hani huruwi kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.

**Kielelezo 3.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 3

### 2.2.2 Swali la 4: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya "Uchumi katika Uislamu" na liligawanyika katika sehemu mbili; (a) na (b) ambapo katika sehemu (a) mtahiniwa alitakiwa kuainisha madhara matatu ya riba na katika sehemu (b) alitakiwa kutoa hoja mbili zinazoonesha jinsi gani atalitatua tatizo la riba.


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 65,330 (97.10%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 35,567 (54.40%) walipata alama 1 hadi 2, na miongoni mwao watahiniwa 17,345 (25.80%) walipata alama 0. Watahiniwa 25,151 (38.50%) walipata alama 1.5 hadi 3, na watahiniwa 4,612 (7.06%) walipata alama 3.5 hadi 5 ambapo miongoni mwao watahiniwa 450 (0.70% ) walipata alama zote 5. Chati namba 4 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi hao kwa asilimia.




***Chati no: 4:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 4*


Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani, kwani watahiniwa 29,763 (45.56%) kati ya 65,330 waliojibu swali hili walipata alama kati ya 1.5 hadi 5. Watahiniwa 25,151 (38.50%) walipata alama za wastani (1.5 hadi 3) kwa sababu walitoa hoja pungufu katika sehemu zote mbili na wengine walijibu sehemu moja na kuacha nyingine. Baadhi yao walijibu sehemu zote mbili lakini maelezo yao hayakutosheleza kupata alama za juu.

Watahiniwa 4,612 (7.06%) waliopata alama za juu (3.5 hadi 5) waliweza kuainisha madhara ya riba kwa usahihi. Waliweza pia kutoa hoja madhubuti kuonesha namna ya kuondokana na tatizo la riba. Watahiniwa hawa walielezea madhara ya riba kuwa ni: *Riba huchafua moyo wa tajiri, riba inamkandamiza mnyonge na mwenye dhiki, riba inaharibu uchumi wa jamii na maendeleo yake, riba ni mali ya dhuluma.* Pia walielezea utatuzi wa tatizo la riba kwa njia mbalimbali kama vile; *Kukopesha bila riba, kushirikiana katika mtaji na kugawana gharama za uendeshaji faida na hasara na kuanzisha benki za Kiislam.* Watahiniwa hawa vilevile walielezea suala la kuielimisha jamii juu ya riba na madhara yake. Kwa ujumla watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipengele cha Uchumi katika Uislamu hivyo waliweza kupata majibu sahihi ya swali hili kwa kuzingatia matakwa ya swali na walipata alama za juu. Kielelezo namba 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri.


4a. Madhara ya riba ni:
i) Ku Riba hudumaza uchumi wa jamii.
ii) Riba hueneza umaskini kwa kasi miongoni mwa watu wa kipato cha chini.
iii) Riba huifanya mali ya mtu kubeba mali za dhulma kutoka kwa wengine, hivyo kupata ghadhabu za Allah (s.w)
4b. i) Kushajihisha watu katika kushikamana na miamala ya Benki za Kiislamu; kwa kufanya hivyo watu watakaa ni wenye kuendesha mali zao bila ya riba yoyote kwani miamala ya Kiislamu inachukia riba.

Kielelezo 4.1 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 4

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa watahiniwa 35,567 (54.40%) walipata alama za chini (0 hadi 1) ambapo miongoni mwao watahiniwa 17,345 (25.80%) walipata alama 0. Watahiniwa hawa walishindwa kuainisha madhara ya riba na kuonesha ufumbuzi wa tatizo la riba. Baadhi yao walibainisha adhabu za Allah (s.w) dhidi ya mtoaji na mpokeaji riba kama vile; *Kuingia motoni, milango ya pepo itafungwa, hataingia peponi, hupata madhambi na kupatiwa adhabu na Mola.* Baadhi ya watahiniwa hawakujibu kabisa swali hili kwakuwa hawakuwa na ufahamu wowote kuhusu majibu ya swali hili. Kwa ujumla watahiniwa hawa walipata alama hafifu na wengine alama 0 kwa sababu ya kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada iliyoulizwa na kutokufahamu matakwa ya swali. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 4 kama linavyotakiwa.



4. a) Madhara matatu ya riba ni yafuatayo
- Mungu kuto mpa hifadhi.
- ~~Kuto~~ ~~wame~~ Allah (s.w) kuto mpa thawabu kwa chochote
anacho fanya kwa riba
- Kuto ~~peke~~ pokelewa dua yoyote ile anayo omba kwa Allah (s.w)

b) Hoja mbili jinsi gani nitalipatia ufumbuzi tatizo la riba.
- Kuacha kutumia mali ya riba
- Kuomba msamaha kwa Allah (s.w) kama hauto tumia tena.

**Kielelezo 4.2** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 4.


### 2.2.3 Swali la 5: Nguzo za Imani

Swali hili lilitoka katika kipengele cha kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu, ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa tofauti kati ya Qudra na Qadar ya Mwenyezi Mungu. Watahiniwa 58,913 (87.50%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 41,608 (70.60%) walipata alama 0 hadi 1. Watahiniwa 15,592 (26.47%) walipata alama 1.5 hadi 3 na watahiniwa 1,713 (2.91%) walipata alama 3.5 hadi 5. Chati namba 5 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hawa kwa asilimia.




**Chati ya: 5:** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 5*


Uchambuzi unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni dhaifu kwani watahiniwa 41,608 (70.60%) kati ya 58,913 waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 1 ambapo miongoni mwao watahiniwa 37,122 (55.20%) walipata alama 0. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha kwa usahihi kati ya Qudra na Qadar ya Mwenyezi Mungu. Hii ilisababishwa na watahiniwa hao kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya nguzo hii ya sita ya Imani. Baadhi ya watahiniwa waliielezea Qudra kuwa ni: *Bahati aliyomjalia mja na Qadar ni makadirio ya mwanadamu aliyokadiriwa, Qudra ni neema anazotoa Allah (s.w) kwenda kwa mja wake na Qadar ni nguzo ya tano ya Uislamu*. Watahiniwa wengine walibuni majibu yao na kuonesha kuwa Qudra ni kinyume cha Qadar. Miongoni mwa majibu hayo ni: *Qudra ni kuamini tofauti na maamrisho ya Allah (s.w) na Qadar ni kuamini kuwa hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah (s.w), Qudra ni maneno yanayosemwa na watu bila kuyatekeleza maamrisho yake na Qadar ni hali ya kutekeleza maamrisho ya Allah (s.w).*Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kipengele hiki cha nguzo za imani hivyo walipata alama hafifu na wengine walipata alama 0. Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi ya swali.


5 Qudra ni dua za mtu kumuomba mungu ku mpangia kitu fulani. Dua za mtu hubadilisha qadar. na
Qadar ni kuamini mwenyezi mungu na siku ya mwisho. Mfano kuamini Qadar, siku ya mwisho.

**Kielelezo 5.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 5

Watahiniwa 15,592 (26.47%) walipata alama za wastani kutokana na kushindwa kutoa maelezo ya kutosha juu ya tofauti iliyopo kati ya Qudra na Qadar ya Mwenyezi Mungu. Baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza maana ya neno moja tu kati ya Qadar na Qudra kwa usahihi hivyo walipata alama za wastani.


Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 1,713 (2.91%) walipata alama za juu (3.5 hadi 5) miongoni mwao watahiniwa 213 (0.30%) walipata alama zote 5. Watahiniwa hawa waliweza kuelezea kwa usahihi tofauti iliyopo kati ya Qadar na Qudra ya Mwenyezi Mungu, kama vile: *Qudra ya Mwenyezi Mungu ni uwezo wake juu ya kila kitu usio na mipaka na Qadar ya Mwenyezi Mungu ni mpango/mpangilio wa kuendesha mambo yote.* Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Nguzo za Imani na walitumia maarifa yao vema kueleza dhana hizo hivyo waliweza kupata alama za juu. Kielelezo namba 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri.


5 Qadar ni mipango ambayo Allah (s.w.) ameipanga ambayo ilisha tokea, itakuja kutokea au inayotokea sasa hivi ambayo Allah kapanga iwe ni kheri au shari hakuna wa kubadilisha mfano siku ya mwisho
Qudra ni Uwezo wa Allah wa kufanya jambo litokee ambapo yeye husema "Kuwa" na mara moja kitu hicho kinakuwa. Mfano Allah alipomuumba mwanadamu alisema kuwa na binadamu akawa.

Kielelezo 5.2 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 5

### 2.2.4 Swali la 6: Nguzo za Uislamu


Swali lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu kipengele cha *Swaumu ya Ramadhani*, na lilimtaka mtahiniwa aorodheshe mambo matano ambayo yanaweza kubatilisha swaumu ya mume na mke katika mchana wa Ramadhani. Watahiniwa 66,422 (98.70%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 35,823 (53.93%) walipata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa 16,683 (25.10%) walipata alama 0 hadi 1 na watahiniwa 13,916 (20.95%) walipata alama 3.5 hadi 5. Chati namba 6 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi hawa kwa asilimia.




***Chati namba 6*** *Kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 6*

Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 49,739 (74.88%) waliojibu swali hili walipata alama kuanzia 1.5 hadi 5 ambazo ni alama za kufaulu kwenye swali hili. Watahiniwa 1,112 (1.70%) walipata alama zote 5. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mada ya Funga ya Ramadhani na walielewa matakwa ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha mambo ambayo yanaweza kubatilisha Funga ya mume na mke kwa pamoja katika mchana wa mwezi wa Ramadhani kama vile: *kula na kunywa mchana wa Ramadhani kwa makusudi, kufanya tendo la ndoa, kujitapisha kwa makusudi kujitoa manii na kunuia kuvunja swaumu*.


Watahiniwa 35,823 (53.93%) waliopata alama za wastani waliezea majibu pungufu kulingana na yaliyohitajika katika kujibu swali hili. Vile vile watahiniwa hawa walichanganya majibu yaliyo sahihi na mengine yasiyo sahihi, kama vile: *Kuamka na janaba, kutokusimamisha swala, matendo maovu, kutokwa na najisi, kusengenya, kutamani, kutooga janaba, kuvaa nguo zinazoonesha, kutotii sharia za Ramadhani, kubusiana mke na mume na kufuata nafsi matamanio.* Kielelezo namba 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


6 i Kufanya tendo la ndoa (jimai) mchana wa Ramadhani.
ii Kula au kunywa kwa makusudi.
iii Kujitoa manii kwa makusudi.
iv Kujitapisha kwa makusudi.
v Kunuia kula au kunywa mchana wa Ramadhani

**Kielelezo namba 6.1** Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 6.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 16,683 (25.10%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi hivyo walipata alama hafifu (0 hadi 1) na miongoni mwao watahiniwa 3,786 (5.60%) walipata alama 0. Hii ni kwa sababu ya kutozingatia matakwa ya swali na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya mambo ya jumla yanayo batilisha Funga ya mume na mke kwa pamoja. Baadhi yao badala ya kuandika yanayo batilisha Funga waliandika mambo ambayo yanadhaniwa kuwa yanabatilisha Funga. Mambo hayo ni kama vile: *kukumbatiana mke na mume, kupigana busu mke na mume, kutamaniana mke na mume, kuamka na janaba na kulia.*

Watahiniwa wengine badala ya kuandika yanayobatilisha Funga, waliandika mambo ambayo yanapunguza uzito au thamani ya Funga, kama vile: *Kusengenya, kutukana, kusema uongo, kuchonganisha, kugombana, kudhulumu, kutosimamisha swala na kutovaa stara*. Kutokana na majibu haya watahiniwa hawa walipata alama hafifu au alama 0. Kielelezo namba 6.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.




| | |
|---|---|
| 6 | Mambo matano yanaoweza kuwaharibia Swaumu |
| i | Kusengenya |
| ii | Kusema Uongo |
| iii | Kufitinisha / Kugombanisha |
| iv | Kutukana |
| v | Kuporoja |

**Kielelezo 6.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 6

### 2.2.5 Swali la 7: Mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu


Swali hili lilitoka katika mada ya mambo ya lazima ya kufanyiwa maiti wa kiislamu. Mtahiniwa alitakiwa kueleza hatua tano za kumkafini maiti wa kiume. Watahiniwa 63,063 (93.70%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 57,238 (90.8%) walipata alama 0 hadi 1. Watahiniwa 5,060 (8.02%) walipata alama 1.5 hadi 3 na watahiniwa 765 (1.21%) walipata alama 3.5 hadi 5. Chati namba 7 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi hao kwa asilimia.




***Chati namba 7:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 7*

Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa dhaifu kwani watahiniwa 57,238 (90.8%) waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 1. Miongoni

mwao watahiniwa 41,561 (61.70%) walipata alama 0, kwa sababu ya kushindwa kuelewa matakwa ya swali na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya namna ya kukafini maiti wa kiislamu. Baadhi ya watahiniwa hawakuelewa na kuandika mambo ya lazima ya kufanyiwa maiti Muislamu badala ya hatua za kukafini maiti wa kiume. Majibu waliyo andika ni: *kuosha maiti, kuvika sanda maiti, kuswalia maiti na kuzika.* Watahiniwa wengine waliandika hatua za kuosha maiti Muislamu kama vile: *Kumfunika maiti kwa nguo yenye kupenyeza maji na kumwagia maji na kumsugua kwa kumgeuzageuza, kumbinya kutoa uchafu tumboni, kumkalisha na kumbinya tena, kumtilisha udhu maiti na kumvalisha sanda.* Watahiniwa wengine walieleza hatua za kumkafini maiti mwanamke badala ya hatua za kukafini maiti wa kiume. Hivyo watahiniwa hawa hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo namba 7.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


7. Zifuatazo ni hatua za kumkafini maiti wa kiume ni:-
i. kumuosha mwili wake wote, hili ni jambo ambalo kila maiti inapaswa kufanyiwa ili aweze kuzikwa vizuri.
ii. kumnyoa nywele zake, maiti ya kiume inapaswa kunyolewa nywele zake za mwilini
iii. kumvisha sanda, maiti ya kiume ina utaratibu wake wa kuvishwa sanda.
iv. kumswali maiti, baada ya hayo ya pili lengine ni kuiswalia maiti kwa [illegible] mungu (S.W)
v. kumzika maiti, hii ni kwa baada ya yote la mwisho ni kumzika katika kaburi lake.

**Kielelezo 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 10

Watahiniwa 5,060 (8.02% ) waliopata alama za wastani (1.5 hadi 2.5) waliweza kutaja baadhi ya hatua bila maelezo ya kutosha juu ya hatua hizo za kumkafini maiti wa kiume na wengine walielezea hatua pungufu ya tano.

Uchambuzi zaidi kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa katika watahiniwa 765 (1.21%) waliopata kuanzia alama 3.5 hadi 5 ni watahiniwa 102 (0.20%) tu walipata alama zote 5 za swali hili. Watahiniwa hawa waliopata alama za juu walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya namna ya kumkafini maiti wa kiislamu. Vile vile walielewa matakwa ya swali, hivyo waliweza kueleza kwa usahihi hatua tano za kumkafini maiti wa kiume kwa kuandika kama vile: *kuweka pande la kwanza la sanda juu ya jamvi, kisha la pili na la tatu, kutoa kamba katika pande zote za jamvi la kwanza, Kamba nyingine zitolewe kwenye jamvi la tatu kwa ajili ya kumfungia maiti ili sanda isije kumvuka akabakia uchi. Maiti alazwe juu ya mapande yote matatu na kuzibwa kwa pamba zilizofukizwa manukato katika matundu yote ya mwili, Maiti atatizwe (afunikwe) kwa mapande yote matatu moja baada ya jingine na kamba zitumike kufunga vitanzi miguuni, tumboni na kichwani*. Kielelezo namba 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali na kueleza kwa ufasaha hatua muhimu katika kukafini.


7. (i) Kukatwa majamvi matatu sawa sawa na kushikizwa kwa uzi kati kati.
(ii) Mashuka kukatwa nyuzi moja kila upande, nyuzi za shuka la kwanza kumfungia kichwani na miguuni, la pili kati na tatu zilizobakia kwa ajili ya kufungia mkeka.
(iii) Kumweka maiti katika majamvi yalio kwisha nyunyiziwa marashi na kupakwa manukato kisha kuanza kumpamba maiti kwa kumtia pamba sehemu zote za viungio. Mfano magotini, na pia sehemu zote za matundu ya mwili mfano puani, ndomoni na machoni.
(iv) Kuanza kumfunga shuka la kwanza, kisha la pili na la tatu na kumfunga kama pipi kwa kutumia nyuzi zilizokatwa kutoka katika mashuka hayo.
(v) Kumfunga maiti mkeka kwa kamba zilizobaki na hapo itakua tayari maiti ya kiume imesha-kafiniwa.

Kielelezo namba 7.2: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 7

### 2.2.6 Swali la 8: Qur`an

Swali hili lilitoka katika mada ya Qur'an, katika mada ndogo ya kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an. Swali lilikuwa na vipengele viwili; (a) na (b). Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa atoe sababu mbili kueleza kwanini Qur'an ilishushwa kidogokidogo na katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kuelezea njia kuu tatu zilizotumika katika kuihifadhi Qur'an.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 64,957 (96.50%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 31,101 (47.88%) walipata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa 30,349 (46.70%) walipata alama 0 hadi 1 na watahiniwa 3,507 (5.40%) walipata alama 3.5 hadi 5. Chati namba 8 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi hawa kwa asilimia.




***Chati namba 8:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 8*


Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa kuwa watahiniwa 34,608 (53.28%) walipata alama 1.5 hadi 5. Watahiniwa waliopata alama za juu walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya Qur'an. Watahiniwa hawa walielewa matakwa ya swali hivyo waliweza kuandika kwa usahihi sababu za kushuka Qur'an kidogo kidogo na njia kuu tatu zilizotumika katika kuihifadhi Qur'an.

Katika kipengele (a) waliandika sababu za kushushwa kidogo kidogo kwa Qur’an kuwa ni: *Ili uthibitishwe moyo wa Mtume (s.a.w) kwa aya mpya, ili kuwa wepesi kwa Mtume (s.a.w) kufikisha ujumbe uliotangulia kwa ukamilifu kabla ya ujumbe uliofuata na ili iwe wepesi kwa waumini wa mwanzo kusoma na kuhifadhi Qur'an.*

Katika kipengele (b) waliainisha njia kuu zilizotumika kuihifadhi Qur'an kama vile: *Kuhifadhishwa Mtume (s.a.w) na kuahidiwa kutosahau, waislamu kuhifadhi Qur'an vifuani mwao baada ya kusomewa na Mtume (s.a.w) na Qur'an kuhifadhiwa katika maandishi chini ya usimamizi wa Mtume (s.a.w).*

Watahiniwa 31,101 (47.88%) walipata alama za wastani kutokana na sababu tofauti tofauti. Baadhi yao walijibu kipengele kimoja tu kati ya (a) na (b) na kuacha kingine badala ya kujibu vipengele vyote viwili. Wengine waliandika hoja pungufu katika kipengele kimoja au vyote viwili.

Sababu nyingine iliyosababisha watahiniwa hawa kupata alama za wastani ni kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi katika vingele vya swali kwa mfano katika kipengele (a) waliandika hoja kama vile: *Hali aliyokuwa nayo Mtume (s.a.w) wakati anapokea wahyi, kutokujua kusoma na kuandika, watu waweze kusilimu, kuaminika Qur'an, kwa sababu Qur'an ni tukufu.* Pia katika kipengele (b) *Mtume aliwaomba waandishi wake wamsomee, kwenye juzuu, kanda, katika mapango na majabali*. Kielelezo namba 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


8 a) i) Ilishushwa kidogokidogo ili iwe rahisi kuhifadhika
ii) Ili kufikisha ujumbe kulingana na matukio
b) i) Mtume alihifadhishwa na Malaika Jibril na Allah S.W.T aliahidi kutomsahaulisha
ii) Mtume aliwahifadhisha masahaba vifuani mwao
iii) Mtume aliteuwa masahaba wapatao 42 ili waweze kuhifadhisha Qur-an katika maandishi na kisha mtume aliwamrisha wamsomee kama ipo sahihi

**Kielelezo namba 8.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8


Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 30,349 (46.70%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1, kati yao watahiniwa 6,171 (9.20%) walipata alama 0. Watahiniwa hawa walijibu kinyume na matakwa ya swali kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada ya Qur'an. Baadhi yao hawakufanya kabisa swali hili katika vipengele vyote viwili (a) na (b).

Watahiniwa wengine waliandika mahali au sehemu ambayo Mtume (s.a.w) alishushiwa Qur'an badala ya kueleza kwa nini Qur’an ilishuka kidogo kidogo kama ilivyoulizwa. Katika majibu yao walielezea: *Qur'an ilishushwa kidogo kidogo Mtume (s.a.w) alipokuwa Jabal Hiraa, Qur'an ilishushwa kidogo kidogo Mtume (s.a.w) alipokuwa anaelekea Makka.*

Kundi lingine la watahiniwa waliofanya vibaya katika swali hili walieleza awamu ama hatua za kushuka kwa Qur’an (kutoka Lauhim mahfudh mpaka wingu wa dunia na kuletwa duniani) badala ya kutoa sababu za Qur'an kushuka kidogo kidogo kutoka wingu wa dunia kuja kwa Mtume (s.a.w). Kundi lingine liliandika kuwa Qur'an kushushwa kidogo kidogo ni Qur'an kushushwa Makka na Madinah.

Katika kipengele (b) kadhalika, baadhi ya watahiniwa badala ya kueleza njia kuu zilizotumika kuhifadhi Qur'an walitoa maelezo kuwa: Qur'an iliandikwa na kuhifadhiwa kwenye: *Magome ya miti, mawe, mapangoni katika mifupa na katika milima mirefu*.

Aidha kuna watahiniwa wengine walijbu kipengele hiki cha (b) kwa kuandika njia anazotumia Allah (s.w) kuwasiliana na waja wake, kama vile: *kutumia malaika, ndoto za kweli na kutumia vibao.* Kielelezo namba 8.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


8(b) Magome ya MtH waislamu walikua wa
kihifadhi Qur-an adi kwenye magome ya
mtH ili wadhi hifadhi.

(ii) Qur-an zilihifadhiwa kwenye majabali
(mawe) makubwa walikua wakihifadhi
Qur-an kwa kusudi ya kuzitunza na kudh
~~tAH~~ ihifadhi kwa jili ya miaka ya baadae
ziweze kutumika.


(iii) Qur-an zilihifadhiwa kwenye mapan
go ndani ya mapango liziweze kutumika
kwa kizazi kingine kisacho.

**Kielelezo 8.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 10

### 2.2.7 Swali la 9: Sunnah na Hadithi

Swali hili lilitoka katika mada ya Sunnah na Hadithi, katika mada ndogo ya uchambuzi wa hadithi za Mtume (s.a.w). Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa aeleze tofauti kati ya Hadithi Qudusy na Hadithi Nabawiyyah na katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa atofautishe Aljar-hi na Ata-adil.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 47,917 (71.20%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 32,412 (67.7%) walipata alama 0 hadi 1. Watahiniwa 14,772 (30.83%) walipata alama 1.5 hadi 3 na watahiniwa 733 (1.53%) pekee ndio walipata alama 3.5 hadi 5. Chati namba 8 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi hao kwa asilimia.




***Chati no: 9:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 9.*


Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 15,505 (32.36%) kati ya 47,914 waliojibu swali hili walipata alama 1.5 hadi 5. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya uchambuzi wa Hadithi za Mtume (s.a.w) hivyo waliweza kutofautisha kwa usahihi baina ya Hadithi Qudusy na Hadithi Nabawiyyah, vilevile Aljar'hi na Ata'adili kwa namna ambayo iliwawezesha kupata alama za juu.

Miongoni mwa tofauti walizozitoa ni kuwa: (a) *Hadithi Qudusyi ni habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kama alivyoipokea kutoka kwa Allah (s.w) ilihali Hadithi Nabawiyyah ni usemi au habari aliyoitoa Mtume (s.a.w) kwa watu kwa maneno yake. Hadithi za aina hii zinaanza kwa maneno amesema Mtume (s.a.w).*

Kipengele (b) *Aljar-hi ni kumtia dosari msimulizi kwa kukataa hadithi yake kutokana na udhaifu aliokuwa nao ilihali Ata-adili ni kumkubali msimulizi wa hadithi kutokana na sifa nzuri alizokuwa nazo.* Kutokana na maelezo haya waliyoyatoa, watahiniwa hawa waliweza kupata alama nzuri.

Watahiniwa 14,772 (30.83% ) walipata alama za wastani (1.5 hadi 3) kwa sababu walijibu kipengele kimoja na kuacha kingine. Vile vile waliandika

maelezo yasiyotosheleza kuhusu istilahi zilizoulizwa. Watahiniwa hawa walipata alama za wastani. Kielelezo namba 9.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutofautisha vipengele hivyo vya Hadithi.


9. Kutofautisha vipengele vya hadithi ifuatavyo:-
a) Hadithi Qudussy ni zile hadithi ambazo matni (maana halisi ya maneno) ni maneno ya Allah (s.w) wakati hadithi Nabawiyyah ni zile hadithi ambazo maana halisi ya maneno (matni) ni maneno ya mtume (s.A.w).
Hadith Qudussy haianzi mara nyingi na maneno ya mtume mwenyewe, ila mtume husema "Allah kasema ~~mtume~~ mtukufu..." au maneno yenye maana hiyo wakati hadithi Nabawiyyah huanzwa na maneno ya mtume au maswahaba huelezea vitendo vyake.

b) Ata-adili ni ile hali ambayo katika hali ya hadithi mtu huwa ni mwadilifu na mwenye kuaminika katika uwanja wa hadithi wakati Aljar-hi ni ile hali ambayo mtu huwa ni mwenye upungufu (mapungufu) ya uadilifu na si muaminifu sana "thiqqah" katika uwanja wa hadithi.

**Kielelezo 9.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 9


Uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 32,412 (67.60%) waliopata alama hafifu (0 hadi 1) walijibu kinyume na matakwa ya swali kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya uchambuzi wa Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w). Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha istilahi walizopewa kama ilivyotakiwa na wengine waliacha kabisa kujibu swali hili.

Baadhi ya watahiniwa hawa walitafsiri neno Aljar-hi na Ata-adil kama aina au tanzu za Hadithi kama vile: *Aljar-hi ni hadithi fupi fupi kutoka kwa Mtume wetu (s.a.w) na Ata-adili ni hadithi ndefu ndefu zenye aya ndefu, Aljar-hi ni hadithi ambayo imesimuliwa na nabii mussa wakati ata-adil ni*

*hadithi ambayo imesimuliwa na nabii Ibrahim na aljar-hi ni hadithi zenye wapokezi wengi wakati at-adil ni hadithi zenye wapokezi kidogo.*

Baadhi ya watahiniwa ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipengele (a) walitoa majibu yafuatayo: *Hadithi qudusy ni hadithi ambayo imepokelewa Makka na mahujaji na nabawiyya ni hadithi ambayo ilipokelewa Madina kwa lengo la kuendeleza uislamu, Qudusy ni hadithi iliyoandikwa enzi za Mtume (s.a.w) na Nabawiyyi ni Hadithi zilizopokelewa na Imamu muslim na Bukhar, Nabawiyya ni hadithi dhaifu na Qudusy ni Hadidhi sahihi na Qudusy ni hadithi za kuhifadhiwa vichwani na hadithi Nabawiyya ni hadithi za kuhifadhiwa kwenye misahafu na juzuu.*

Wengine katika kujibu kipengele (a) walifananisha Hadithi Qudusy na Nabawiyah kama vile Hadithi Mutawatir na Ahad na kuzieleza kama; *hadithi qudusy ni hadithi ambayo imesimuliwa na watu wachache wakati Nabawiyyah ni hadithi ambayo imesimuliana watu wengi*. Kutokana na majibu haya na mengine yanayofanana na hayo watahiniwa hawa walipata alama hafifu au alama 0. Kielelezo namba 9.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


9 (a) Hadithi Qudusy – Ni adisi toka kwa imamu Bukhari,
na Hadithi Nabawiyyah – Ni kutoka kwa imamu Shaffii
(b) Aljar-hi – Hadithi Zinazo mahusu mtume Muhammad,
na Ata-adili – Hadithi Zinazo wahusu manabii wengine
mfano Ibbrahimu (A.S).

**Kielelezo 9.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 10


## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Kila swali lilikuwa na alama 15**.** Jumla ya alama katika sehemu hii ilikuwa 45. Maswali katika sehemu hii yalitoka katika mada za: Dola ya Kiislamu Madina, Qur an, Nguzo za Uislamu na Mfumo wa jamii ya Kiislamu.

### 2.3.1 Swali la 10: Dola ya Kiislamu Madinah

Swali hili lilitoka katika mada kuu ya Dola ya kiislamu Madinah katika kipengele Kutawafu kwa Mtume (s.a.w). Watahiniwa walitakiwa kueleza mafunzo manne wanayopata Waislamu kuanzia kuumwa hadi kutawafu kwa Mtume Muhammad (s.a.w).

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 45,147 (67.10%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 27,210 (60.30%) walipata alama 0 hadi 4.5. Watahiniwa 16,501 (36.55%) walipata alama 5 hadi 9.5 na watahiniwa 1,436 (3.18%) walipata alama 10 hadi 15 za swali hili. Chati namba 10 inaonesha kufaulu kwa wanafunzi hao katika asilimia.




***Chati 10:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 10*


Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 17,937 (39.73%) kati ya watahiniwa 45,147 waliojibu swali hili walipata alama 5 hadi 15. Watahiniwa waliopata alama za juu waliweza kubainisha mafunzo sahihi kutokana na kuugua hadi kutawafu kwa Mtume (s.a.w). mafunzo hayo ni kama vile: *Ugonjwa sio sababu ya mtu kuacha kufanya ibada na majukumu mengine, kiongozi anapopata dharura sio sababu ya mambo kusimama bali akabidhi mtu mwingine majukumu yake, tunafundishwa kuwa ni bora maiti*

*ashughulikiwe na ndugu zake wa karibu kinasaba na uchungu wa umauti utampata kila mtu akiwa mwema au muovu.* Kielelezo namba 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa usahihi mafunzo yatokanayo na kuugua hadi kutawafu kwa Mtume (s.a.w).

10 Mtume Muhammad (s.a.w) ni mtume wa mwisho wa Allah (s.w) aliyeletwa ulimwenguni na kushushiwa kitabu kitakatifu cha Qur-an ili kiwe kipambanuzi baina ya haki na batili pia muongozo. Mtume alianza kuumwa mara tu baada ya hija ya kuaga na kutawafu katika mji mtakatifu wa Madinah. Yafuatayo ni mafunzo wanayoyapata waislamu kuanzia kuumwa mpaka kutawafu kwa Mtume (s.a.w).

Kifo ni jambo lisiloepukika kwa kila binadamu kwani hata kipenzi cha mungu alikufa. Mtume (s.a.w) alitawafu katika mji wa ~~Makka~~ Madina mara baada ya kuugua na kutangazwa na swahaba wake kuwa ametawafu na kwa yeyote aliyekuwa akimuabudu ajue kuwa ametawafu na wanaomuabudu Allah (s.w) basi yu milele. Hivyo tunajifunza pia ya kujiandaa na mlango huu ambao kila binadamu ataupitia kwa njia yake kulingana na matendo yake.

Kupigania dini ya Allah (s.w) na kusimama katika misingi ya haki na sheria hadi mwisho wa maisha yetu. Waislamu wanapata funzo la kupigania dini ya uislamu na kusimama katika misingi ya haki na sheria ya kiislamu kama Mtume alivyokuwa akiipigania dini hii katika kipindi chote cha uhai wake alikuwa mzima hadi anakufa katika misingi imara ya dini ya kiislamu kwani hakuonekana kuwa dhaifu katika suala ya kupigania dini hata wakati anaumwa kwani alisimamia mambo ya ibada katika msikiti kwa kumchagua imamu kwa niaba yake aliyeongoza swala. Hivyo tunajifunza kupigania dini ya Allah mpaka mwisho.



10 Kuendeleza ibada ni lazima na muhimu hata kama muislamu ni mgonjwa. Mtume Muhammad (s.a.w) alipokuwa anaumwa hakuacha kuswali hata mara moja na alihakikisha kuwa ibada ya jammah inaendelezwa msikitini kwa kumchagua Abubakar (r.a) kuwa kiongozi pale ambapo alizidiwa sana. Hivyo kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) ni kigezo chetu huyo tunajifunza kuwa waislamu hawana budi kuendeleza ibada kama vile swala kwa nyakati zake hata kama ni mgonjwa.

Maradhi ni sababu mojawapo ya kifo hivyo waislamu wanapopatwa na maradhi wamshukuru na kumdhikiri Allah (s.w) kwani ni nusra kwa wamchao Mwenyezimungu. Kifo cha mtume Muhammad (s.a.w) kilisababishwa na maradhi aliyokuwa nayo mwilini mwake pia waislamu huweza kupatwa na maradhi na kuwa sababu ya kifo cha muislamu huyo. Ni nusra kwa wamchao Allah (s.w) pia tunahimizwa kumshukuru kwa Qadar hiyo na kumdhikiri kila wakati ili kufaulu kwelikweli. Kama mtume alivyoendeleza dhikri kwa Allah hata pale alipopata fwa na maradhi hivyo tunajifunza kutokana na hilo.

Hakika mtume Muhammad (s.a.w) ni kigezo chema kwetu sisi waislamu hivyo hatuna budi kufuata yale aliyokuwa akiyafanya na kuacha yale yote aliyotukataza kuyaacha pia kumpenda ikiwa ni pamoja na kumswalia sana pale anapotajwa na hata mwezi kutakujengea ari ya kuiga mwenendo wake katika kuelekea kila kipengele cha maisha yetu hivyo kufaulu hapa duniani na Akhera.

**Kielelezo namba 10.1** Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 10

Watahiniwa 16,501 (%) walipata alama za wastani (5 hadi 9.5) kutokana na kushindwa kutoa maelezo ya kutosha katika hoja walizozianisha ingawa hoja zao zilikuwa sahihi. Wengine walitoa hoja pungufu ya nne ambazo zilihitajika katika swali hili. Watahiniwa wengine walichanganya majibu


sahihi na yasiyo sahihi kama vile: *Imani ya kweli, malipo mazuri ni kutoka kwa Allah (S.W), kuamini qadar, tunajifunza kuwa Allah (S.W) ni Muweza wa kila jambo na Allah (S.W) ndiye aliyemtuma Mtume (s.a.w).*

Watahiniwa 27,210 (60.30%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi hivyo walipata alama hafifu (0 hadi 4.5) ambapo miongoni mwao watahiniwa 3,246 (4.8%) walipata alama 0. Hii ni kwa sababu ya kushindwa kujua matakwa ya swali na wengine kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya historia ya kutawafu kwa Mtume (s.a.w).

Baadhi ya watahiniwa walionesha kuwa hawakuelewa kabisa matakwa ya swali kwani waliorodhesha vitendo vya waja wema kama mafunzo kutokana na tukio hili, mfano wa majibu hayo ni kama vile: *uvumilivu, uchamungu, subra, kufanya mambo mema kuutangaza Uislamu, kumuamini Mwenyezi Mungu, kusoma Qur'an kiufasaha, kujua jinsi ya kuishi na jirani na kujipamba na tabia njema*.

Watahiniwa wengine walielezea sifa na uwezo wa Mwenyezi Mungu kama mafunzo, mfano: *Allah (s.w) ni Mola wa viumbe vyote humchukua amtakaye, Allah (s.w) humnusuru amtakaye, Allah (s.w) ndiye mwenye mamlaka ya kufanya chochote na Allah (s.w) humpa amtakaye na kumnyima amtakaye.*

Baadhi ya watahiniwa badala ya kuandika mafunzo ya tukio hili, walieleza sifa za Mtume (s.a.w) kama ilivyozoeleka kwa jamii kumsifia kiongozi anapofariki, kama vile: *alikuwa na mapenzi makubwa na watu, alikuwa mwaminifu, alikuwa mkarimu, alikuwa mchamungu na alikuwa akitoa zakat sadaka.* Kwa ujumla watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa juu ya mada hii na wengine hawakuelewa kabisa matakwa ya swali, hivyo baadhi yao walipata chini ya alama tano (5) huku wengine wakipata alama 0. Kielelezo namba 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kama inavyostahili.



Kutawafu ni kitendo ambacho kinafanywa na watu kwa kuzunguka Al-kaaba mara saba kuanzia jiwe jeusi. Yafuatayo ni mafunzo manne wanayoyapata waislamu kuanzia kuumwa ~~kwa mtume~~ mpaka kutawafu kwa mtume Muhammad (s.a.w) kama ifuatavyo:-

Tumejifunza maana ya kutawafu: Funzo moja wapo ni hili ambalo waislamu wameyapata kwa kwenda kutawafu miongoni mwa wanaadamu.

Tumejifunza kuwa mtume muhammad (s.a.w) ni mtume wa mwenyezi mungu. Pia ndio funzo tulipata wakati wa kuumwa mpaka kutawafu kwa mtume muhammad (s.a.w)

Maana halisi ya kutawafu: Ndio nyenzo kuu katika maisha ya mwanadamu wa kiislamu.

Kufikana na kuumwa kwa mtume.

Kufikana na mafunzo manne yaliyopo hapo juu, hayo ni mafunzo ambayo tunayapata waislamu kuanzia kuumwa mpaka kutawafu mtume muhammad (s.a.w).

10 Kuolo za mafunzo manne waneyoyapata Waislamu kuanzia kumuwa ~~na~~ mpaka kuta wafu kwa Mtume Muhammad (S.a.w) mambo hayo ni:

Kumwamini Muumba Mungu kauwa yupo; Waislamu tunapata mafunzo kuanzia kumuwa mpaka kutuwafu kwa Mtume Muha mmad (S.a.w) kwa Muumba Mungu yupo hapo tunapata funzo kuteka kwa Mtume wafu Muha mmad (S.a.w)

Kuamini vitabu vya Muumba Mungu; Waislamu tunapata mafunzo kuanzia kumuwa na mpaka kutuwafu kwa Mtume Muhammad (S.a.w) kwa kupata funzo la kuamini vitabu vya Muumba Mungu.

Kuamini mitume wa Muumba Mungu; Waislamu tunapata mafunzo Kuanzia kumuwa mpaka kutuwafu kwa Mtume Muhammad (S.a.w) kwa kuamini mitume wa Muumba Mungu

Kuamini siku ya mwisho; Waislamu tunapata mafunzo kuanzia na mpaka kutuwafu kwa Mtume Muhammad (S.a.w) kwa kuamini siku ya mwisho katika ulimwengu huu tunaamini kwa siku ya mwisho ipo tangu kumuwa na kutuwafu kwa Mtume Muhammad (S.a.w)


Kwa kumaliza mafunzo waliyoyapata Waislamu kuanzia kumuwa na mpaka kutawafu kwa Mtume Muhammad (S.a.w) ni kumwamini Muumba Mungu, kuamini vitabu vyake na mambo mengineyo Waislamu walipata

**Kielelezo namba: 10.2** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 10

### 2.3.2 Swali la 11: Qur'an.

Swali hili lilitoka katika mada ya Qur'an, katika mada ndogo ya kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze namna Mtume (s.a.w) alivyoteremshiwa Qur'an kwa mara ya kwanza na kueleza mafunzo manne yanayopaswa kufanyiwa kazi katika maisha ya kila siku kutokana na tukio hilo.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 48,693 (72.30%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 28,239 (58.00%) walipata alama 0 hadi 4.5. Watahiniwa 18,973 (39.0%) walipata alama 5 hadi 9.5 na watahiniwa 1,481 (3.04%) walipata alama 10 hadi 14.5. Chati namba 11 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hawa kwa asilimia.




***Chati namba 11:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 11*

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 20,454 (42.01%) kati ya 48,693 waliojibu swali hili walipata alama 5 hadi 14.5. Watahiniwa waliopata alama za juu (10 hadi 14.5) waliweza kueleza kwa umahiri namna Mtume (s.a.w) alivyoteremshiwa Qur'an kwa mara ya kwanza na kubainisha mafunzo manne yanayopaswa kufanyiwa kazi katika maisha ya kila siku kutokana na tukio hilo. Watahiniwa hawa walieleza kuwa: *Mtume (s.a.w) alianza kushushiwa Qur'an mwaka 610 A.D akiwa na umri wa mika 40 katika pango la Jabal Hira katika usiku wa mwezi wa Ramadhani. Malaika Jibril*

*alimuendea mtume pangoni hapo na kumuamuru asome. Mtume (s.a.w) alijibu kuwa hajui kusoma. Jibril alimbana kwa nguvu na alipomuachia alimsomea aya tano za mwanzo za suratul Alaq. Mtume alirejea nyumbani na aya hizi huku akitetemeka kwa hofu na alimuhadithia mkewe Bi Khadija yote yaliyompata.* Mafunzo waliyoyatoa kutokana na tukio hili ni pamoja na: *Elimu ni amri ya kwanza aliyopewa mtume (s.a.w), kutafuta elimu sio jambo jepesi bali tutakumbana na magumu mengi, utukufu wa Mwezi wa Ramdhani unatokana na Qur'an kuanza kushuka mwezi huo hivyo tuzidishe kusoma Qur'an katika mwezi huo na Qur'an ni kitabu cha Allah (s.w).*

Watahiniwa 18,973 (38.96% ) walipata alama za wastani (5 hadi 9.5) kwakuwa hawakutoa maelezo ya kutosha juu ya historia ya kushushwa kwa Qur'an kwa mara ya kwanza na mafunzo tunayoyapata. Baadhi ya watahiniwa waliandika hoja pungufu ya nne na walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi kama vile: *Kutekeleza maamrisho na kuacha makatazo, tunapaswa kufuata sharia na kanuni, tunapaswa kumuamini Allah (s.w) na Mtume wake, Jibril ndiye aliyekuwa akishusha wahyi na kutii amri Allah (S.w) ni sababu ya kupata radhi zake.* Kielelezo namba 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


11 Qur-an ~~imes~~ ni kitabu alichoshushiwa Mtume Muhammad kupelekea ujumbe kwa watu zake. Mtume (s.a.w) aliposhushiwa kitabu hichi alikuwepo pangoni ambalo likiitwa Jabal thawri. Hali aliyokuwa nayo Mtume (s.a.w) wakati anashushiwa kitabu hichi ili kuwa si ya kawaida ambapo mtume aliogopa mpaka akakimbia kwa mkewe Bi Aisha na ndipo ilipoteremshwa Suratul Mudathir. Mtume (s.a.w) alipata tabu sana wakati akishushiwa wahyi huo na kuupokea kutoka kwa Jibril ambapo ni amri ya Allah (s.w).

Miongoni mwa mafunzo tunayoyapata katika maisha ya kila siku kupitia tukio hilo ni:

Tunatakiwa tutekeleze amri ya Allah (s.w). Hii inamaanisha kwamba waislam tunatakiwa tufuate amri na tuache kila tunachokatazwa ili kunusurika na adhabu ya Allah hii inafungamana na pale Jibril alipompa amri Mtume Muhammad asome na kufuata amri.

Pia Tunajifunza kwamba jambo la Elimu ni jambo la mwanzo analotakiwa mwanadamu kutafuta. Hii inamaana ya kwamba suala la elimu limehimizwa katika uislam wote wanawake na wanaume. kama Jibril alivyomhimiza Mtume suala la kusoma wakati anashushiwa Qur-an.

Pia tunajifunza kwamba tusikate


tamaa na kumkufuru wakati tanatafuta
elimu. Hii inamaana ya kwamba muisla
m anatakiwa ajitolee kutafuta elimu na
si kumkufuru mola wake wakati anapota
futa. Hilo linafungamana na pale Mtume
(s.w) alipobinywa mbavu wakati anaposome
shwa Qur-an na Jibril na mwishowe
kuja kujua kama inavyotakikana.
Pia tunapaswa kuamini kwamba Qur-an
ni maneno ya Allah na si ya Mtume (s.w). Hii
ni kwa sababu na hali aliyokuwa nayo waka
ti akiteremshiwa. Kwa hiyo tunapaswa
tuisome kwa ajili ya kupata radhi za
Allah.
Hivyo basi hayo ni miongoni mwa
mafunzo tulijifunza wakati Qur-an ina
teremshwa kwa mara ya kwanza na kufa
radhishwa kwa elimu.

**Kielelezo namba 11.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 11

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 28,239 (58.00%) walipata alama hafifu (0 hadi 4.5) ambapo miongoni mwao watahiniwa 2,455 (3.60%) walipata alama 0. Watahiniwa hawa walijibu kinyume na matakwa ya swali kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya historia ya kushushwa na kuhifadhiwa kwa Qur'an.

Baadhi ya watahiniwa hawa badala ya kueleza namna Mtume (s.a.w) alivyoshushiwa Qur'an kwa mara ya kwanza na mafunzo tunayoyapata kutokana na tukio hilo waliandika majibu ya jumla yaliyokuwa kinyume na matakwa ya swali kama vile, hali aliyokuwa nayo Mtume (s.a.w) baada kupokea wahyi, kwamba: *Alikuwa mwoga sana baada ya kumuona Jibril, baada kushushiwa Qur'an alikuwa anatetemeka, Mtume (s.a.w) alibadilika haiba, Mtume (s.a.w) alipewa jukumu la kufundisha Qur'an na alikuwa hajui kusoma wala kuandika*.

Watahiniwa wengine waliandika faida za kuisoma Qur'an na kuifuata kama vile: *Qur'an ni kinga kwa mwanadamu, Qur'an inamfanya Mtu kuwa mchamungu, Qur'an humrahisishia mtu kufanya jambo, Qur'an inamfanya mtu kuwa muadilifu, Qur'an inafanya waislamu kushirikiana, Qur'an inapelekea watu kuwa na hofu juu ya Allah (S.W) na Qur'an imepelekea kuvumbuliwa kwa Sunnah.*

Kwa ujmla watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa juu ya historia ya kushushwa kwa Qur'an, hivyo baadhi yao walipata alama hafifu na wengine walipata alama 0. Kielelezo 11.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa kuzingatia matakwa ya swali.

11 Mtume aliyoteremshiwa quran kwa mara ya kwanza na Allah alihifadhi na kuwasomea maswahaba hao wahifadhi na waandike kama walivyo hifadhishwa na kusomewa na mtume.
Zifuatazo ni mafunzo yanayopaswa kufanyi wa kazi katika maisha ya kila siku kutokana na tukio hilo.
Humuwezesha mja kusoma akiwa twahara na kuanza kumlaani shetani. funzo tunalolipata hapo niku wa mtume aliyoteremshiwa quran na Allah alihifadhishwa kama wahyi kutoka kwa Allah kwa sababu alikuwa ajui kusoma na kuandika na yeye akawasomea maswahaba zake iliwaandike kama walivyosomewa kwa hiyo funzo tunalolipata hapo tunatakiwa kusoma quran tukiwa twahara na tukiwa na udhu na kabla ya kusoma quran tunatakiwa kwanza tumlaani sheetani kwanza ndipo tusome qur-an na kuhifadhi kama mtume (s.a.w).

11 Humuwezesha mja Kuwa Kuanza na bismillahir na Kuwa mnyenyekevu wakati wa Kusoma; hili ni funzo tunalopata wakati wa Kusoma quran baada ya ya Kumlaani shetani tunatakiwa Kusema ~~na~~ Bismillahir na Kuwa mnyenyekevu wakati wa Kusoma tunatakiwa tuwe wanyenyekevu wakati wa Kusoma quran tunatakiwa tuwe na heshima wakati wa Kusoma quran na tuanza na Kusema bismillahir ni Kumsifu mwenyezi mungu tunatakiwa tuwe na heshima wakati wa kusoma quran.

Humuwezesha Kusoma quran Kwa sauti nzuri na Kuzingatia maana ya Kila aya; hili ni funzo tunalolipata wakati wa kufanyiwa kazi katika maisha ya Kila siku Kutokana na tukio hilo inatubidi Kuweza Kusoma quran vizuri na Kwa sauti nzuri Kwa Kuzingatia maana ya Kila aya katika maisha ya Kila siku tunabidi Kusoma quran Kwa sauti nzuri na Kuweza Kusoma maana ya Kila aya unayoisoma inabidi uyuKutokana na tukio hilo la ku Kuteremshwa quran.

Kutekeleza maamrisho yake na Kujizuia na makatazo yake; hili ni funzo la mwisho tunalopata Kufanyiwa Kazi quran katika maisha ya Kila siku Kutokana na tukio hilo inatubidi tutekeleze maamrisho yake na Kujizuia na makatazo yake ni Kuamba inatubidi tu fuata sheria na masharti yaliyo elekezwa ndani ya quran. Hili ni funzo la namna mtume (s.a.w) aliyoteremshiwa quran Kwa mara ya Kwanza na Kisha Kupata mafunzo Kufanyiwa Kazi Katika maisha ya Kila siku.


Hivyo basi Kutokana na tukio hilo tunapata mafunzo aliyoteremshiwa quran Kwa mara ya Kwanza na Kufanyiwa kazi katika maisha ya Kila siku.

**Kielelezo namba 11.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 11

### 2.3.3 Swali la 12: Nguzo za Uislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya Nguzo za Uislamu katika mada ndogo ya kusimamisha Swala za jamaa. Mtahiniwa alitakiwa kueleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kuandaa Khutba ya Ijumaa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 32,967 (49.00%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 25,356 (76.90%) walipata alama 0 hadi 4.5 za swali hili. Watahiniwa 4,988 (15.13%) walipata alama 5 hadi 9.5 na watahiniwa 2,623 (7.96%) walipata alama 10 hadi 15. Chati namba 11 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hao katika asilimia.




***Chati namba: 12:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 12*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa dhaifu, kwakuwa watahiniwa 25,356 (76.90%) kati ya 32,967 waliofanya swali hili walipata alama 0 hadi 4.5 ambapo miongoni mwao watahiniwa 9,369 (13.90%) walipata alama 0. Watahiniwa hawa walijibu kinyume na matakwa ya swali kwa sababu ya  kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya khutuba ya Swala ya ijumaa, hususani nguzo zake, badala ya kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa khutuba ya Ijumaa watahiniwa wakaelezea hatua za

kufuata katika kufikisha khutuba ya Ijumaa, kama vile: *salamu na utangulizi, mwanzo wa hutuba, kiini au katikati ya khutuba na mwisho wa khutuba au hitimisho*. Watahiniwa wengine walifahamu kuwa mambo ya kuzingatia kabla ya kuandaa khutuba ni namna khatibu anavyotakiwa kuwa au sifa za khatibu na khutuba yenyewe, hivyo wakatoa sifa kama vile: *Khatibu awe na udhu, awe nadhifu, awe mnyenyekevu, awe amehifadhi Qur'an na kuielewa, awe amehifadhi Hadithi na kuzielewa, awe anajua tafsiri ya sura zote na awe amehifadhi tafsiri ya Hadithi zote.*

Na katika sifa za khutuba wakaeleza kuwa: *Khutuba iwe fupi nzuri na yenye kueleweka, khutuba itumie lugha ya walengwa, khutuba ilenge jamii husika, khutuba ilenge matatizo ya jamii, isiwe ya kusengenya mtu, isiwe na utata na izingatie muda.* Pamoja na kuwa baadhi ya mambo waliyoyaeleza ni ya kweli lakini sio majibu sahihi kwa sababu sio nguzo za khutuba ya Ijumaa, hivyo watahiniwa hawa walipata alama hafifu na wengine alama 0. Kielelezo namba 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa kuzingatia matakwa ya swali.


12. Khutba ya Ijumaa ni maneno yatolewayo na kiongozi fulani yaliyobeba ujumbe mahusus wenye kuhimasisha moma na kukataza maboya kabla na baada ya swala ya jamaa (rakaa mbili) za Ijumaa. Khutba hii hubeba rakaa mbili za swala na baraka tele hivyo yafuatayo ni mambo matano ya kuzingatia wakati wa kuandaa Khutba ya Ijumaa.

Urefu; Wakati wa kuandaa khutba ya Ijumaa urefu ni jambo la muhimu sana kwasababu watu wengi wali'o wa Islamu wameacha biashara zao ama familia zao hivyo Khutba hiyo inabidi iwe fupi yenye kueleweka ili kupunguza mda zaidi wa swala hiyo na kuweza kuendelea na mambo mengine ya uzalishaji.

Mada; ni lazima wakati wa kuandaa Khutba ya Ijumaa kiongozi ajue kabisa ni jambo gani mahusus analo kwenda kuzungumza mbele ya jamii ya Kiislamu siku hiyo siyo kwenda na kuanza kuzungumza chochote ajisikiacho hapana lazima kiwe mahususi na kiongozi awe anafahamu analotaka kuzungumza.

Ujumbe: Wakati wa kuandaa khutba ya Ijumaa ni vyema ujumbe uwe wenye kuelimisha jamii nzima kwa yakini hivyo basi kiongozi anapaswa kujua ujumbe huo anao utoa kwa hadhira ni wenye kuikomboa jamii juu ya jambo fulani mfano: Madhara ya zinaa katika jamii ni ya kudhalilisha hivyo hii hurahisisha watu kupata ujumbe haraka kabla khutba kuisha.

Rika; Kiongozi huyu wakati akiandaa khutba ya Ijumaa lazima aandae khutba ambayo inawagusa waislamu wa rika zote na kuweza kujifunza kutokana na khutba hiyo iliyotolewa. na pia khutba hiyo inatakiwa kwa na ujumbo wa kugusa jamii nzima kwa hakika ili iweze kukomboa jamii yote ya Kiislamu.




**Kielelezo namba 12.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 12

Watahiniwa 4,988 (15.13%) waliopata alama za wastani (5 hadi 9.5) walikuwa na mapungufu mbalimbali kama vile: Baadhi walitaja majibu sahihi lakini hawakutoa maelezo kamili juu ya mambo hayo. Wengine walieleza pungufu ya mambo matano yaliyohitajika na baadhi yao waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kama vile: *kutoa salamu kwa waislamu, kuwaruhusu waislamu kuomba dua, kuweka kituo baina ya khutuba mbili, kuwa na mfano wa aya na hadithi, lugha ya khutba ifanane na wale wanaohutubiwa, mada iendane na jamii na khutuba iwe ni yenye kuelimisha*. Baadhi ya mambo haya ni kweli hufanyika wakati wa khutuba ya Ijumaa lakini sio katika misingi ya kuandaa khutuba ya Ijumaa.

Uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,623 (7.96%) walipata alama za juu ambapo miongoni mwao watahiniwa 7 walipata alama zote 15 za swali hili, watahiniwa hawa walionesha kuelewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya uandaaji wa khutba ya  Swala ya Ijumaa.

Watahiniwa hawa waliweza kueleza kwa usahihi mambo matano ya kuzingatia wakati wa kuandaa khutuba ya Ijumaa kuwa ni: *Kuanza khutuba ya Ijumaa kwa kumhimid au kumshukuru Allah (s.w,), kisha kumswalia au kumtakia rehema na Amani Mtume (s.a.w), kuwausia waislamu juu ya kumcha Allah (S.w), kusoma aya au sura yeyote katika Qur'an na kuwaombea waislamu/waumini wote dua.* Kielelezo namba 12.2

kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


12. Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa khutba ya Ijumaa.

Khutba ni maneno anayo sema imamu kwa waumini wake ili kuwakumbusha lengo lao la kuletwa hapa duniani na kuwafundisha / kuwakumbusha juu ya maamrisho na makatazo ya Mwenyezimungu. Ili khutba ya Ijumaa ikamilike lazima kuwepo na mambo ya kuzingatia ili kuweza kukamilisha khutba hiyo. Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa khutba ya Ijumaa.

Kumhimidi Allah; Mhutubu anapotaka kutoa khutba ni lazima aweze kumhimidi Allah (kumpwekesha Allah) kwani Allah ndiye aliyemuumba na sifa zote anastahili Allah (s.w) kwa kuwa yeye ndiye muumbaji wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Hivyo basi kabla mtoaji khutba hajaendelea na khutba anatakiwa kumpwekesha Allah. kwanza hilo ni jambo muhimu la kuzingatia wakati wa kuandaa khutba.

Kumtakia rehma Mtume Muhammad (s.a.w); Pia muandaaji wa khutba anatakiwa kuhakikisha kuwa anamtakia rehma Mtume Muhammad kwani katika uandaaji wa khutba jambo la pili baada ya kumhimidi Allah ni kumtakia rehma Mtume Muhammad (s.a.w) kwani yeye ndiye kiongozi wetu wa zama zetu.

Kutoa nasaha kwa waislamu; Pia jambo la kuzingatia ni kuwanasihi waislamu kwani hapa mtoaji wa khutba anapata nafasi ya kuweza kuwahusia waislamu juu la suala zima la kuumbwa kwao na pia kuwaelimisha juu ya masuala wasio yajua juu ya dini yao na hapa ndipo muhutubu anaweza kuwanasihi juu ya mafundisho na makatazo ya Mtume Muhammad (s.a.w).



Kusoma Qur-an walau aya moja; Katika uandishi wa khutba lazima mkhutubu atakapo mataja vipengele hivyo vya mwanzo ambavyo ni kumhimidi Allah, kumtakia rehma Mtume Muhammad (s.a.w) na kuwausia waumini pia anatakiwa kusoma qur-an ili kuweza kuwatia imani waislamu wale hata aya moja.

Kuwaombea dua waislamu na wake wale kwa ujumla; Pia khutba ili iweze kutimia lazima iwe na vipengele hivi vitano ambavyo. katika vipengele hivyo mtoaji wa khutba anatakiwa awaombee dua waislamu wote na wake wengine kwa ujumla endapo kipengele kimoja wapo kati ya hivi kitapungua basi khutba itakuwa haijatimia kwani kila kipengele kina umuhimu wake.


Hitimisho: Muandishi wa khutba anatakiwa kuzingatia kuwa kila kipengele kinatakiwa kufuatwa kwani endapo kitapungua hata kipengele kimoja wapo basi khutba hiyo itakuwa haijatimia.

**Kielelezo namba 12.2:** Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 12

### 2.3.4 Swali la 13: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu

Swali hili lilitoka katika mada ya Mfumo wa jamii ya Kiislamu katika mada ndogo ya Sheria katika Uislamu. Mtahiniwa alitakiwa afafanue kazi tano za sheria ya Kiislamu katika jamii.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 56,876 (84.50%) kati ya watahiniwa 67,309 waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 34,211 (60.20%) walipata alama 0 hadi 4.5 za swali hili. Watahiniwa 19,454 (34.20%) walipata alama 5 hadi 9.5 na watahiniwa 3,211 (5.65%) walipata alama 10 hadi 15. Chati namba 13 inaonesha kufaulu kwa watahiniwa hawa katika asilimia.




***Chati namba 13:*** *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 13*

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 22,665 (39.85%) kati ya 56,876 waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 5 hadi 15.

Watahiniwa waliopata alama za juu (10 hadi 15) walielewa vema matakwa ya swali na walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya sheria katika Uislamu. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha kazi za sheria ya kiislamu katika jamii kama vile: *Kumlinda mwanadamu dhidi ya madhara yanayoweza kusababishwa na mwenendo wake mbaya, kulinda watu na mali zao, kuhifadhi maadili ya jamii, kuhifadhi amani na usalama, kupanga utaratibu namna ya kuendesha shughuli mbalimbali zenye maingiliano ya kijamii na kulinda na kuhifadhi dini.*

Watahiniwa 19,454 (34.20%) waliopata alama za wastani (5 hadi 9.5) hawakutoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu kazi tano za sheria ya kiislamu ingawa walizitaja kazi hizo kwa usahihi. Baadhi ya walitaja walitaja kazi pungufu ya zile zilizohitajika katika swali na wengine waliandika kazi tano za sheria za Kiislamu huku wakizirejea hoja zao kwa maneno mbadala na kuziandika kama hoja mpya.

Watahiniwa wengine waliachanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi ndani ya insha moja, kama vile: *kujenga jamii mpya, kutoa hukumu ya mambo mbalimbali, kutatua juu ya migogoro na kuwaongoza waumini katika lengo la kuumbwa.* Kutokana na sababu hizi, watahiniwa hawa walipata alama za wastani. Kielelezo namba 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.

(13)

masharti,
Sheria ni taratibu, masuala na kanuni
zilizo wekwa kwaajili ya kushughulikia
maingiliano ya watu katika jammii na kila
mtu anatakiwa azifuate. Katika dunia sheria
zigawanyika katika sheria za kitwaghuti ambazo
chimbuko lake ni fikera za watu katika uendeshaj
i wa shughuli na sheria za kiislamu ambazo chim
buko lake ni Quran, Sunna na Ijitihad. Katika sheria
za kiislamu ifuatazo ni kazi zake katika jamii ya
kiislam ambazo ni;
kwanza Sheria ina kazi madhubuti
ya kulinda mali na watu jamii fukani. Hii ina
maanisha kwamba katika Sheria ya kiislamu
moja wapo ya misingi yake Quran imeelezea
haki ya binadamu kulindwa na si yoyote yule
isipokuwa Allah (sw). Sheria hivyo basi inatuonye
sha ~~[illegible]~~ umuhimu wa kulinda watu kupitia
msaada wa Allah. Pia sheria inakazi ya kulinda ma
li ya watu kwa maana amana zake mfano - Quran
imeelezea kuwa haki za umilikaji wa mali pamo
ja na maelezo ya mtume (saw). Hivyo basi sheria
inalinda mali na watu katika kama ilivyoelezewa.
Bakora
ii) Sheria inakazi ya kusimamisha
haki na uadilifu katika jamii. Ina maana kwa
mba sheria inasimamisha haki bila ya upendele
o wa Hadhi, ubaguzi wa Rangi na kha kadhalik
a kwa mfano - Sheria ya kiislamu imeelezea
kuwa mzinifu anahaki ya adhabu ya Bakora
mia moja na mlevi (Bakora themanini). Hivyo

Sheria za kiislamu haina upendeleo bali ipo kat
ika msimamo madhubuti katika kusimamisha
haki katika jamii zetu za kiislamu.

Sheria ina kazi ya kuhifadhi maadi
li ya jamii. Hii inamaana kwamba sheria
za kiislamu zimeweka makatazo katika mi
momonyoko wa maadili mfano - Uislamu ume
keza sheria kupitia Quran kwa tabia zina
zoharibu maadili kama zinaa, ulevi zinama
katazo yake na hukumu zake na kuachana
kupunzia swala za mumini aliyo elekeza mtu
me(saw) na Mola wake Allah(sw).

Bali pia, Sheria za kiislamu zinakata
zi ya kuweka na kusimamisha Amani na
Busara katika jamii. Katika Quran na mafun
disho ya mtume zimekatazwa upiganaji ambao
unaondoa amani na busara katika jamii am
bazo huweza kusababisha vita katika jamii
na uislamu umekataza upiganaji ambao ni vita
bila za kikafiri.

Alafu Sheria ina kazi ya kusimamia
na kuongoza shughuli mbali mbali ambazo zi
na mwingiliano ya kibinadamu katika jamii
haswahasa kwa mfano katika masuala ya
kimahakama, Hakimu anafuata sheria kulinga
na na uislamu unavyoelekeza. Katika mahakam
a taratibu zinafuatwa katika njia zifuataz
wo kutuhumiwa bila hatia, upelelezi, haki ya
mtuhumiwa kusikiliza kesi na kujieleza na
haki ya kuachiliwa na mfungwa.

Hitimisho ni kwamba sheria ni muh
imu sana katika jamii, inasaidia kulindama

adili ya mwanadamu mfano swala, pia ina
saidia kulinda haki za watu na kusimamis
ha uadilifu katika jamii bila upendeleo kwa
mujibu wa mafundisho ya mtume(saw) na All
ah(sw) katika Quran na sunnah.

Kielelezo 13.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 13

Uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 34,211 (60.20%) walipata alama hafifu (0 hadi 4.5) kati yao watahiniwa 6,860 (10.20%) walipata alama 0. Watahiniwa hawa walijibu kinyume na matakwa ya swali, kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya sheria katika Uislamu na kazi zake katika jamii.

Watahiniwa hawa badala ya kuandika kazi ya sheria ya Kiislamu katika jamii waliandika makatazo mbalimbali ya sheria ya Kiislamu kama vile: *sheria inakataza kuiiba, sheria inakataza kuzini, sheria inakataza kuuwa, sheria inakataza riba, sheria inakataza kufanya maovu.* Kwa ujumla watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kazi za msingi za sheria ya Kiislamu katika jamii. Watahiniwa wengine walieleza maamrisho ya sheria ya Kiislamu kama vile: *kusoma Qur'an, kufunga ramadhani, kusimamisha swala, kutenda mema na kuwa mtiifu kwa kazi yeyote.*

Baadhi ya watahiniwa walibadilisha maudhui ya swali kutoka kazi tano za sheria ya Kiislamu na kuelezea kama nguzo tano za Uislamu, kwa hiyo walifafanua nguzo tano za Uislamu badala ya kazi za sheria ya Kiislamu katika jamii. Watahiniwa wengine katika kundi hili walijitunga majibu yasiyohusiana na mada ya sheria katika Uislamu kama vile masharti ya utoaji Zakat na Sadakat wakichanganya ndani yake nguzo za Uislamu, kwa mfano: *kuwapa wanaostahiki, kutoa vilivyo halali, kwenda kuhiji makka, kutoa zakat na kufunga ramadhani.* Kielelezo namba 13.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kama ilivyotakiwa.


13 Sharia ni Maamrisho ya uislamu aliyoyatoa allah kwa waja wake. Ziqatazo ni Kazi za sheria ya Kiislamu katika jamii.

Kulingania dini ya kiislamu, hii ni sheria ya Kiislamu katika jamii; kuilingania dini ya kiislamu kwa waislamu.

Kuaminisha waja juu ya Kuwepo kwa allah, hii ni kazi ya sheria ya Kiislamu katika jamii ya Kuaminisha waja juu ya Kuwepo kwa muumba kwa kuwatolea aya za wibitisho mfano kuwepo kwa usikunamchana kuumbwa kwa mbingu na ardhi na kufa na ~~mfano~~ wa kuwepo kwa siku ya mwisho.

Kuelimisha juu ya umuhimu wa ndoa za Kiislamu, hii ni kazi ya sheria za kiislamu katika jamii; kwa kuelimisha juu ya umuhimu wa ndoa kwa sababu ya kupunguza dhinaa watoto wa nje ya ndoa ~~na~~

Kuelimisha juu ya mavazi ya kiislamu kwa waume na wake katika jamii kwani dunia yetu ya sasa


13 Waumini kwa kwa wake hawajui ni mava-
zi gani waliyo halalishiwa na kuharami-
shiwa kwa mfano Mke amehalalishiwa
kuvaa vazi linalofanana na ba mume
pia mume amehalalishiwa kuvaa vazi
linalo onyesha uchi wake.
Kutoa mafunzo ya swala
kwani watu wengi at wanasasa tunaona
hawapo katika kumuabudu allah hivyo
wakitoa mafunzo ya swala watafuata
na kumuabudu allah.
Kuelimisha juu ya kuhiji
huko makkah, kuna baadhi ya waumini
hujua kuwa wanaoenda kuhiji ni wale
wenye uwezo kumbe sio hivyo kuhiji
ni kwa mtu yeyote unaweza kufanya
biashara ndani ya miaka miwili ukawa
na lengo la kwenda kuhiji na Mungu
akakuwezesha ila tu usitafute kwa
njia ya haramu.
Hivyo basi hizi ni sharia
za kiislamu katika jamii tunatakiwa
kuzijua na kuzifanyia kazi.

**Kielelezo 13.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali la 13

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwaka 2019 ulikuwa na jumla ya maswali 13 ambayo yalitungwa kutoka katika mada kumi na moja (11) ambazo ni: *Dola ya kiislamu Madinah, Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w), Sunnah na Hadithi, Qur'an, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Familia ya Kiislamu, Mfumo wa Jamii ya Kiislamu, Nguzo za Uislamu, Mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu, Sheria katika Uislamu na Nguzo za Imani*.

Mada zilizotahiniwa katika swali la kwanza ni: *Dola ya Kiislamu Madinah, Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w), Sunnah na Hadithi, Qur'an, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Familia ya Kiislamu, Sheria katika Uislamu na Nguzo za Imani* ambazo kwa ujumla watahiniwa walifanya vizuri na kufaulu kwa asilimia 95.42.

Uchambuzi wa takwimu wa matokeo ya watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu katika mada zifuatazo: *Nguzo za Uislamu* (50.76%), *Qur'an* (47.64%), *Mfumo wa Jamii ya Kiislamu* (42.71%), *Dola ya Kiislamu Madinah* (36.55%), *Familia katika Uislamu* (34.20%) na *Sunna na Hadithi* (32.36%). Kiwango hiki cha kufaulu kilitokana na: Watahiniwa kujibu maswali kwa maelezo yasiyojitosheleza, kutotimiza idadi ya vipengele vilivyotakiwa kujibiwa kwenye maswali na kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi katika majibu yao.

Aidha mada zilizokuwa na kiwango cha chini cha kufaulu ni: *Nguzo za Imani* (29.37%) na *Mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu* (9.24%). Uchambuzi uliofanywa umebaini kuwa sababu kubwa za mada hizi kuwa na kiwango cha chini cha kufaulu ni watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha na kushindwa kuelewa matakwa ya maswali.

Muhtasari wa uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa kwa mada umeoneshwa kwenye kiambatisho ambapo rangi nyekundu inaonesha kiwango hafifu cha kufaulu, rangi ya njano inaonesha kufaulu kwa wastani na rangi kijani inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu katika swali husika.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa wa Elimu ya Dini ya Kiislaamu kidato cha nne mwaka 2019 ni cha wastani (43.29%). Uchambuzi huu umeonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa ili kuboresha kiwango cha kufaulu. Aidha changamoto zilizobainika ni kama vile: Watahiniwa kutofuata maelekezo ya swali hivyo kushindwa kutoa majibu yanayojitosheleza; Kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi; Kutoa maelezo yasiyojitosheleza kwa hoja sahihi walizozitoa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali.

Ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu kwenye mada zote katika mitihani ijayo jitihada zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea watahiniwa uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali, namna ya kuyajibu kwa usahihi, na kuboresha namna ya kuwasilisha hoja kwa maandishi katika muundo wa insha au majibu mafupi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, mambo yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu waboreshe ufundishaji wa mada kwa kuwaongoza wanafunzi katika vikundi kueleza namna ya kutekeleza haki za maiti Muislamu.

(b) Walimu waboreshe ufundishaji wa mada kwa kuwaongoza wanafunzi kivitendo au kwa kutumia igizo kuonesha namna ya kutekeleza haki za maiti Muislamu.

(c) Walimu waboreshe ufundishaji kwa kuwaongoza wanafunzi kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu kueleza dhana (istilahi) mbalimbali za kiitikadi na kubainisha umuhimu wake.

## 6.0 Kiambatisho

UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

| Na. | Mada | Kufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya wanafunzi waliopata wastani wa alama 30 au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nambari ya Swali | Asilimia ya Kufaulu | | |
| 1 | Dola ya Kiislamu Madinah, Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w), Sunnah na Hadithi, Qur'an, Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Familia ya Kiislamu, Sheria katika Uislamu, Nguzo za Imani. | 1 | 95.42 | 95.42 | Vizuri |
| 2 | Nguzo za Uislamu | 2<br>6<br>12 | 50.76 | 58.46 | Wastani |
| 3 | Qur'an | 8<br>11 | 47.64 | 48.12 | Wastani |
| 4 | Mfumo wa Jamii ya Kiislamu. | 4<br>13 | 42.71 | 42.71 | Wastani |
| 5 | Dola ya Kiislamu Madinah | 10 | 39.73 | 39.73 | Wastani |
| 6 | Familia katika Uislamu | 3 | 34.20 | 34.20 | Wastani |
| 7 | Sunnah na Hadithi | 9 | 32.36 | 32.36 | Wastani |
| 8 | Nguzo za Imani | 5 | 29.37 | 29.37 | Dhaifu |
| 9 | Mambo ya lazima kufanyiwa maiti Muislamu. | 7 | 9.24 | 9.24 | Dhaif |
| **Wastani wa Jumla wa Kufaulu** | | | | **43.29** | **Wastani** |